HOTUBA YA MH. ENG. EVARIST NDIKILO MKUU WA MKOA WA PWANI KWENYE KILELE CHA MAADHIMISHO YA SIKU YA UKIMWI DUNIANI YANAYOFANYIKA KIMKOA KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA BAGAMOYO TAREHE MOSI DESEMBA, 2020

- *Dkt. Delphine Magere, Katibu Tawala Mkoa wa Pwani,*
- *Mhe.Zainabu Kawawa,Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo,*
- *Wahe. Wabunge: Mhe. Mkenge (Bagamoyo) na Ridhiwani Kikwete (Chalinze),*
- *Viongozi wa Kamati ya Amani Wilaya,*
- *Mhe. Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo na Chalinze,*
- *Ndugu Makatibu Tawala Wasaidizi wa Mkoa,*
- *Katibu Tawala wa Wilaya ya Bagamoyo,*
- *Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Bagamoyo,*
- *Waheshimiwa Madiwani,*
- *Watumishi wote wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Halmashauri,*
- *Wadau Mbalimbali,*
- *Waandishi wa Habari*
- *Wageni waalikwa,*
- *Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana,*

Ndugu Wananchi,

Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutukutanisha mahali hapa tukiwa wazima na wenye afya njema. Aidha, nitoe shukrani za pekee kwa Viongozi, Wadau na wananchi wote wa Wilaya ya Bagamoyo kwa kukubali kubeba jukumu la kuwa mwenyeji wa Maadhimisho haya ya Siku ya UKIMWI Duniani kwa Mwaka huu wa 2020, yanayofanyika Kimkoa hapa Bagamoyo. Napenda pia kuwashukuru nyote kwa kunipa heshima ya kuwa Mgeni Rasmi katika maadhimisho haya. Ahsanteni sana. Aidha, niwapongeze vikundi vyote vilionesha bidhaa mbalimbali, huduma mbalimbali kwa jamii, ushuhuda n.k. Nimefarijika na yote niliyoyaona na kusikia. Pongezi kwa asilimia 10 ya Halmashauri ya Wilaya.

Ndugu Wananchi,

Umoja wa Mataifa uliamua siku ya tarehe 01 Desemba ya kila mwaka kuwa siku ya Kimataifa ya Maadhimisho ya UKIMWI Duniani. Lengo la Maadhimisho haya ni kupima na kutathmini kiasi cha utekelezaji wa malengo na maazimio mbalimbali kuhusu Mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI. Aidha, siku hii hutumika kwa malengo MATATU yafuatayo:-

1. Kuhamasisha na kuelimisha jamii juu ya namna ya kujikinga na maambukizi mapya ya VVU,

2. Matumizi sahihi ya ARV kwa watu wanaoishi na VVU pamoja na

3. Kupinga unyanyapaa na ubaguzi.

Ndugu Wananchi,

Kauli mbiu ya Maadhimisho ya Siku ya UKIMWI kwa mwaka huu 2020 ni ***"Mshikamano wa Kimataifa, Tuwajibike kwa Pamoja" (Global Solidarity, Share Responsibility).*** Kaulimbiu hii inasisitiza ushiriki na ushirikishaji wa Kimataifa, Kitaifa na Jamii katika shughuli za udhibiti wa VVU na UKIMWI kuanzia kwenye upangaji mikakati, upatikanaji wa rasilimali na utoaji wa huduma za VVU na UKIMWI kwa makundi yote ya wanaume, wanawake, vijana walio katika umri wa balehe wenye umri wa miaka 15-24, akinamama wajawazito na wanaonyonyesha pamoja na watoto wao kwa upimaji wa afya zao.

Ndugu Wananchi,

Wakati Dunia ikiadhimisha Siku hii ya UKIMWI ambayo leo ni Miaka 41 iliyopita tangu ugundulike rasmi duniani, kila mmoja wetu akumbuke kwamba VVU na UKIMWI bado upo na achukue hatua za makusudi ya kupambana na janga hili, kwa kuwa hakuna dawa ya kuponya UKIMWI pia hakuna CHANJO. Hali halisi ya maambukizi ya VVU na UKIMWI Kitaifa yanapungua. Takwimu za Utafiti wa Viashiria vya VVU na UKIMWI nchini wa mwaka 2016-2017 vimeonyesha kushuka kwa kiwango cha

maambukizi kutoka asilimia 7 ya mwaka 2003 mpaka kufikia asilimia 4.7. Hali hii inaonesha mafanikio makubwa katika Mapambano Dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI nchini. Kiwango cha maambukizi kwa Mkoa wa Pwani kimepungua kutoka asilimia 5.9 ya mwaka 2012 hadi asilimia 5.5 kwa mwaka 2017 ingawa bado tupo juu ya wastani kitaifa.

Ndugu Wananchi,

Tunazo Halmashauri 3 za Kibaha Mji, Mkuranga na Chalinze bado zinaonekana kuwa na maambukizi mengi kutokana na uwepo shughuli nyingi za mwingiliano wa kiuchumi kwa mfano uwepo wa Viwanda vingi, maeneo mengi ya Kibiashara, vituo vya magari makubwa n.k. Niwaombe viongozi wa Wilaya zote kuweka Mikakati mahususi ya kudhibiti maambukizi mapya ya VVU.

Ndugu Wananchi,

Ushamiri wa maambukizi mapya ya Virusi vya UKIMWI miongoni mwa Wanaume, Wanawake na Vijana wenye umri kati ya miaka 15 – 49 ni mkubwa. Kwa mwaka 2020 yaani kuanzia (Januari – Novemba) maambukizi kwa wanaume yalikuwa **3,667** kati ya wanaume **101,534** sawa na asilimia **3.6** Kwa Wanawake maambukizi yalikuwa ni **5,725** kati wanawake **134,357** waliopima maambukizi ya VVU sawa na asilimia **4.3**. Kwa upande wa vijana kuanzia miaka 15-24 kwa kipindi cha Januari

hadi Novemba, 2020 kiwango cha maambukizi mapya ni **1,396** kati ya **83,049** sawa na asilimia **1.7.**

Katika suala zima la upimaji wa hiari, idadi kubwa ya wanaopima ni wanawake ukilinganisha na wanaume. Kwa mwaka yaani kuanzia 2020 (Januari hadi Novemba) wanaume waliohudhuria katika Vituo vya kutolea Huduma za Afya ni **306,486** na kati yao waliopima VVU ni **101,534** sawa na asilimia **33,** ikilinganishwa na Wanawake **382,193** waliohudhuria, ambapo **134,357** walipima sawa na asilimia **36.**

Kwenye Huduma ya Matunzo na Tiba, jumla ya watu wanaoishi na Virus vya UKIMWI walioandikishwa hadi kufikia Novemba 2020 ni **45,573** ambapo kati ya hawa walioanza dawa ni **9,249** na waliopo kwenye dawa ni **44,950** na kuna watoro **19,041**. Uwepo wa watoro kiasi hiki si ishara nzuri katika mapambano dhidi ya UKIMWI, kwa sababu hiyo, naomba sana Halmashauri ziendelee kutoa elimu ya ufuasi mzuri wa dawa.

Ndugu Wananchi

Kama sehemu ya Mapambano hayo WAVIU pia hupima wingi wa Virusi, kwa hiyo, hadi Novemba, 2020 jumla ya WAVIU **34,590** wamepata huduma ya kupima wingi wa Virus vya UKIMWI na kati yao **31,943** sawa na asilimia **92.4** wamepata ufubavu wa VVU. Hii ni ishara nzuri kwani inaonyesha kuwa afya zao zinaendelea vizuri. Niwasihi sana WAVIU

wasibweteke na kufubazwa kwa VVU na kuanza mienendo isiyofaa na lazima tuendelee kufuata maelekezo ya wataalam ili kulinda afya zetu

Ndugu Wananchi,

Katika kudhibiti Maambukizi ya VVU kumekuwa na changamoto mbalimbali ambazo zinasababisha kuendelea kuwepo kwa maambukizi. Baadhi ya changamoto zinazochochea Maambukizi ni zifuatazo: Mila potofu katika jamii, Ndoa za utotoni, kuwepo vituo vya Maegesho ya Malori kwenye barabara kuu, Ulevi uliopindukia, ngoma za usiku (vigodoro), Wagonjwa kutoka nje ya Mkoa hususani kutoka Jiji la Dar es Salaam, Maeneo hatarishi ya starehe, kuwepo makundi maalumu hatarishi ya watu kama vile Biashara ya ngono (madada poa) na watu wanaojidunga Madawa ya Kulevya. Aidha idadi ndogo ya vituo vya kutolea huduma ya kufubaisha VVU, Umbali wa vituo vya kutolea huduma za Afya na makazi ya watu, kukosekana kwa mashine ya kupima wingi wa Virusi vya UKIMWI katika Mkoa. Hizo ni miongoni mwa changamoto zinazokwamisha juhudi za mapambano dhidi ya UKIMWI.

Ndugu Wananchi,

Katika juhudi za Mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI, Mkoa ulizindua Kampeni ya “**FURAHA YANGU**” mwezi Septemba, 2018. Lengo la uzinduzi

wa kampeni hii ambayo kaulimbiu yake ilikuwa ni '**PIMA, JITAMBUE, ISHI'** ni kuona wananchi wa Mkoa wa Pwani wanatambua hali zao za maambukizi ya VVU, hususani wanaume na makundi mengine ambayo ni Wasichana walio katika umri wa balehe, Wanawake vijana wenye umri wa miaka 15-24, akinamama wajawazito na wanaonyonyesha pamoja na watoto wao.

Mkoa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali waliopo ndani na nje ya Mkoa ulifanya mapitio ya Mpango Mkakati wa UKIMWI wa mwaka 2015 hadi 2020. Lengo la mkakati huu ni kupunguza na kuondoa viashiria vinavyosababisha maambukizi ya VVU, hivyo Halmashauri zilishauriwa kuwa na sheria ndogo za kudhibiti sherehe na shughuli mbalimbali zenye viashiria vya Maambukizi ya VVU mfano Vigodoro. Halmashauri pia, zinatakiwa kuendelea kutoa Elimu ya Kujikinga na maambukizi ya VVU ili kutengeneza mazingira ya mtu kujitambua zaidi. Wataalamu wanaojishughulisha na upimaji wa VVU wanatakiwa kuwa na lugha ya staha kwa wapimwaji ili kutokuwakatisha tamaa. Ninaziagiza Kamati za kata na vijiji/mitaa kufanya kazi za kuhamasisha kujitolea ili kupunguza maambukizi mapya ya UKIMWI. Aidha kila palipo na mkusanyiko wa watu na sherehe kutolewe ujumbe wa tahadhari ya kujikinga na UKIMWI kabla ya kuanza kwa shughuli hiyo. Serikali ya Mkoa inawaomba wadau

mbalimbali wanaoshughulika na Masuala ya Kudhibiti UKIMWI kuendeleza jitihada hizi.

Ndugu Wananchi,

Napenda kuhitimisha kwa kuwakumbusha kwamba UKIMWI bado ni Janga la Taifa na Kimataifa na la KIDUNIA, hivyo ni vyema kila mmoja kuwa na wajibu wa kuchukua tahadhari stahiki na kuendeleza mapambano dhidi ya Maambukizi ya Virusi vya UKIMWI. Tukumbuke A:B:C: katika maisha yetu ya kila siku, viongozi wa DINI mtanisamehe katika hili. Sisi Serikali lazima tuseme ukweli na wananchi wetu.

Mwisho ninawashukuru tena kwa maandalizi mazuri na ushirikiano wenu mlionyesha katika maadhimisho haya. Ninaomba Mungu aendelee kutulinda ili tusafiri salaam tunaporejea nyumbani.

PWANI BILA MAAMBUKIZI MAPYA YA UKIMWI, INAWEZEKANA.

ASANTENI KWA KUNISIKILIZA